



# Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Simu: +255 26 - 2963822  
Nukushi: +255 26 - 2963828  
Barua pepe: dg@nbs.go.tz  
Tovuti: www.nbs.go.tz

Barabara ya Jakaya Kikwete  
S. L. P. 2683  
**DODOMA**  
**TANZANIA**

## TANGAZO LA KAZI ZA WADADISI (NAFASI 34)

Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) inawatangazia watanzania wenye sifa kuomba **kazi ya muda** ya udadisi au ukusanyaji wa takwimu nafasi 34 kwa ajili ya Utafiti wa **SERVICE DELIVERY POINTS** utakaofanyika katika maeneo yatakayochaguliwa Tanzania Bara kwa kipindi cha muda usiozidi miezi miwili.

Waombaji wanatakiwa kuwa ni watanzania wenye sifa zifuatazo;

**a) Sifa za Msingi:-**

- i. Umri wa miaka 18 na kuendelea,
- ii. Cheti cha astashahada (certificate) au stashahada (Diploma) ya Taaluma ya Uguzi,
- iii. Elimu ya kuanzia Kidato cha Nne,
- iv. Cheti cha usajili au leseni ya kufanyakazi ya Taaluma ya Uguzi,

**Nakala za vyeti vya taaluma na vyeti vya kidato cha nne/sita vithibitishwe na Hakimu au Wakili**

**b) Sifa za Ziada:-**

- i. Cheti cha Ujuzi wa kutumia Kompyuta,
- ii. Uzoefu wa kazi ya kukusanya takwimu katika tafiti mbalimbali za afya

Barua za maombi ziandikwe kwa mkono wa mwombaji akionesha anuani kamili na namba yake ya simu pamoja na kuambatisha nakala ya vyeti vyote vya elimu, mafunzo na wasifu wa mwombaji (CV).

Kwa watumishi wa umma maombi yao yapitie kwa waajiri wao ili yaweze kupata kibali.

Barua ya maombi ya kazi yatumwe kwenye Ofisi ya Taifa ya Takwimu - Makao Makuu (Dodoma) kabla ya **tarehe 21 Septemba, 2018** kupitia anuani ifuatayo;

Mkurugenzi Mkuu,  
Ofisi ya Taifa ya Takwimu,  
S.L.P 2683,  
**DODOMA**

**NB:** Wale watakaochaguliwa kwa ajili ya usaili huu ndio watakaoitwa. NBS haitahusika na gharama za kuja Dodoma kwenye usaili huu,

IMETOLEWA NA  
MKURUGENZI MKUU  
OFISI YA TAIFA YA TAKWIMU  
13 SEPTEMBER, 2018